

شَفَاعَةُ الرَّحْمَنِ  
وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آتَيْنَا مِنْكُمْ وَمَكَلِّفُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَخْلِفُوهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَنْسَخْنَا  
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُمْ بِئْرٌ أَرْضُنَا لَهُمْ وَلَمْ يَجِدُوهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقَهُمْ أَثْنَانًا  
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ



Toleo: 1445 / 10

Jumamosi, 2 Dhu al-Hijjah 1445 H

08/06/2024 M

### Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Hizb ut Tahrir / Tanzania Yafanya Visimamo vya Kuyataka Majeshi ya Waislamu Kuiokoa  
Gaza

#### (Imetafsiriwa)

Kufuatia kamjeni ya Hizb ut Tahrir / Tanzania inayoendelea dhidi ya mauaji ya halaiki, ukatili, maumivu na dhalma za Waislamu wa Gaza zinazofanywa kinyama na umbile vamizi la Kiyahudi kwa uungaji mkono wa Marekani na mataifa mengine ya Magharibi.

Hizb ut Tahrir / Tanzania ilifanya visimamo baada ya swala ya Ijumaa (7 Juni 2024) katika sehemu mbalimbali kukemea ukatili wa umbile la Kiyahudi na kuwasilisha suluuhisho la Kiislamu juu yake.

Wazungumzaji katika visimamo hivyo mbali na kulaani kamjeni hiyo ya mauaji ya umbile la Kiyahudi kwa Waislamu wa Gaza, pia wamewakumbusha na kuwataka Waislamu haswa majeshi ya ulimwengu wa Kiislamu kusonga mbele mara moja kuwaokoa Waislamu wa Gaza kwani ulinzi wa maisha ya Waislamu ni faradhi muhimu ya Mwenyezi Mungu kwani ilisisitizwa na Mtukufu Mtume (saw) katika mwezi kama huu (Dhu al-Hijjah) katika Hija yake ya Kuaga.

Visimamo vinne vilifanyika katika jiji la Dar es Salaam nje ya Msikiti wa Lindi na Msikiti wa Idrissa yote ikiwa huko Kariakoo, Msikiti wa Kichangani huko Magomeni na Msikiti wa Dar es Salaam huko Kigamboni. Pia vyengine vilifanyika katika mikoa ya Mtwara na Mwanza.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) Aharakishe Nusra (ushindi) Wake kwa Gaza na Waislamu wote wa mashariki na magharibi - Amin.

Masoud Mselleem  
Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir  
Tanzania